

## **Itikadi za Kisiasa Katika Vitabu Teule vya Fasihi ya Watoto ya Kiswahili**

**John M. Kobia, Ph.D.  
Chuo Kikuu cha Chuka**

**Na  
Faith Muthoni Nyaga  
Chuo Kikuu cha Chuka**

Makala hii inachunguza itikadi za kisiasa zinavyojitokeza katika vitabu teule vya fasihi ya watoto ya Kiswahili kwa kurejelea *Usininyonye* (Komora, 1971), *Zimwi la Leo!* (Wamitila, 2002) na *Sungura Mpanda Ngazi* (Kobia, 2008). Makala hii inaongozwa na Nadharia ya Umaksi. Mihimili ya nadharia ya Umaksi ilizingatiwa katika uchambuzi wa hadithi teule. Data iliyopatikana ilichanganuliwa kwa mbinu elezi kwani ilikuwa data ya kinathari. Matokeo ya utafiti huu yalibainisha kuwa fasihi ya watoto si fasihi ya kitoto kwani inashughulikia masuala ya kisiasa na maendeleo endelevu.

**Maneno makuu:** Itikadi, Siasa, Fasihi ya Watoto, Fasihi ya Kiswahili, Maendeleo endelevu.

Email: [jkobia2001@yahoo.com](mailto:jkobia2001@yahoo.com)0720809725